



### **Madaktari, Sikika wakutana na Katibu Mkuu CCM**

Leo tarehe 14/05/2019 Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) na taasisi ya Sikika wamekutana na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally ofisini kwake Dodoma. MAT iliwakilishwa na rais wake Dk. Elisha Osati na Sikika iliwakilishwa na Mkurugenzi wake Mtendaji Bw. Irenei Kiria.

Ajenda kuu ya mkutano huo ilikuwa kujadili uhusiano na mawasiliano kati ya wanasiasa na watoa huduma za afya, bajeti ya afya na changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya afya Tanzania.

Katika mazungumzo hayo, Dk. Bashiru alieleza kusikitishwa kwake na matukio ya wanasiasa kuingilia utoaji huduma za afya na kudhalilisha watoa huduma. Aliueleza ujumbe huo kwamba hakuna mtu anayewatuma wanasiasa kufanya hivyo na kuwataka wadau wote kushirikiana kwa kuwalinda wataalamu wa wafya na kuwakinga dhidi ya udhalilishaji.

Katibu Mkuu aliahidi kwamba CCM iko tayari kushirikiana na wataalam wa afya kutengeneza mazingira bora ya ushirikiano kati yao na wanasiasa ili kuwahudumia wananchi ipasavyo. Ili kuondoa mgongano huo, Dk. Bashiru aliwataka wadau wa afya kutengeneze mkakati wa kutoa elimu ya namna bora ya mawasiliano kati ya wanasiasa na wataalamu wa afya.

Pia Dk. Bashiru ameshauri kuchapisha orodha ya mambo yanayotakiwa na yasiyotakiwa kufanywa na wadau mbalimbali wanapokuwa katika mazingira ya hospitali na kisha kuyasambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Vile vile, ameshauri kuundwa jukwaa litakalojumuisha wanataaluma wa afya, watafiti kutoka vyuo vikuu, pamoja na asasi za kiraia. Lengo ni kusaidia kutafsiri tafiti kwenda kwenye uhalisia, kutoa elimu ya afya kwa wananchi na ushauri wa kisera kwa serikali.

Taasisi hizo zilimuomba Katibu Mkuu wa CCM awasisitize wanasiasa kuwatangazia zaidi wananchi kiasi cha fedha zinazotolewa na serikali kuliko fedha zilizotengwa. Hii itasaidia kukuza uelewa na kuzuia migongano kati ya wanasiasa na wanataaluma kwa upande mmoja, na watoa huduma na wananchi kwa upande mwingine.

Mambo mengine yaliyozungumziwa ni pamoja na mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya afya, sera ya msamaha wa matibabu kwa makundi mbalimbali na umuhimu wa kila mtanzania kuwa na Bima ya Afya. Mazungumzo hayo pia yaligusia changamoto za rasilimali watu katika utoaji wa huduma za afya, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, majengo na miundombinu.

MAT na Sikika pia walielezea kuridhishwa kwao na juhudi zinazoendelea kufanyika katika sekta ya afya, ikiwemo kuboresha huduma za kibingwa na ujenzi wa vituo vya afya.

Imetolewa na;

Dk. Elisha Osati, Rais wa MAT

Bw. Irenei Kiria, Mkurugenzi wa Sikika